

Learning by Ear 2010

Theme: Illiteracy and education

“A GIRL FINISHING SCHOOL”

Episode 06: “*Latifa afuata njia-mkato.*”

Author: Frédéric GAKPARA

Editor: Yann Durand

Translator: Anne Thomas

Characters:

Latifa (*Ana umri wa miaka 15. Ni binti yao Papa Wali and Mamoua. Mwaka wa tisa huu anaosoma. Ni mwerevu kiasi kwamba hajawahi kurudia darasa lolote. Hata hivyo anakabiliwa na tatizo la wazazi wake kutaka kumwachisha masomo wakati anapojiandaa kufanya mtihani.*)

Zakia (*Ana umri wa miaka 20, ni msichana aliye na uhuru wa kujitendea mambo, ni rafiki yake Latifa na ameajiriwa katika afisi ya wakala wa Utalii kutokana na tajriba yake ya kimasomo. Ni msichana aliyebahatika kutembelea mahali pengi na hukutana na watu wengi kazini mwake.*)

Elinam (*Ana umri wa miaka 19, ni mwanao Papa Wali na Mamoua, ni kaka yake Latifa. Hivi karibuni amejiunga na chuokikuu katika jiji kubwa kilomita kiasi 120 kutoka mji mdogo wanakoishi wazazi wake*)

Roland (*Mwanamume mwenye umri wa miaka 28, mtalii wa Kizungu aliyevutiwa si haba na Zakia. Zakia hampi mwanamume huyo nafasi!*)

Mamoua (*Mwenye umri wa 39, mke na mama ya watoto wa Papa Wali. Ni mjamzito wa mtoto wao wa nne. Hajui kusoma na kuandika. Anafanya biashara ndogo ya kuuza uji wa unga wa mahindi mbele ya nyumba yao.*)

INTRO

Hujambo na karibuni kwenye kipindi cha Noa Bongo-Jenga Maisha Yako katika sehemu ya tatu ya mfululizo wetu wa “Mtoto wa kike ahitimu shule” unaoelezea elimu na kutojua kusoma na kuandika.

*Latifa ameanza likizo yake vizuri. Biashara ya Papa Wali nayo imeanza kustawia. Ziada ya hayo, Papa Wali ameondokea kuwa akifuata ushauri wa Epiphane, mfanyikazi wake. Masomo yake ya jioni yamemuwezesha Epiphany kuvumbua mbinu za kuimarisha biashara yao. Watalii wa Zakia, wanaotafuta bidhaa za kienyeji, hawatatizwi na bidhaa za Papa Wali zilizotengezwa kwa wa mikono. Mambo yameanza kutengemaa nyumbani kwani Papa Wali sasa ndiye anayeulipa mkopo wa Mamoua. Maisha yanaendelea kuwa mazuri! Kwa muda wa siku mbili sasa, Latifa amekuwa akiruhusiwa kuandamana na Zakia pamoja na watalii wake. Ni wakati wa chakula cha mchana na wote wanakula chakula pamoja kwenye mkahawa ulio mlimani. Hii ni sehemu ya sita iitwayo: **Latifa afuata njia-mkato.***

Scene 1, AT THE RESTAURANT ON THE MOUNTAIN

Zakia, Latifa, Roland, Elinam akizungumza kwa simu...

1. SFX ATMO: OPEN-AIR RESTAURANT. WIND IN THE TREES. BIRDSONG. CHILDREN PLAYING. SOUND OF CUTLERY AND CROCKERY. MORE TOURISTS VOICES

2. Zakia: Latifa, inaonekana bado unaota wewe.

3. **Latifa:** Sivyo hivyo! La hasha, Zakia! Mahali hapa panavutia ajabu. Utadhani unaota!
4. **Roland:** Amesema kweli – hapa mahali ni kama peponi.
5. **Zakia:** Asante sana Roland! Ni sehemu muhimu sana kwa kampuni yetu. Tunajitahidi kuitunza kwa kila hali ili watalii wengine kama wewe wafaidi. Lakini majangili pamoja na wanavijiji wanaotafuta kuni wanatutaliza kwa kiasi kikubwa. Mara nyingine wanawasha moto inayowatatiza wanyama. Haifai kwa kweli!
6. **Roland:** Jee wanajua kwamba ni mahali panapolindwa?
7. **Zakia:** Bila shaka, wanalijua hilo! Wanakuja hapa kwasababu hakuna doria inayofanywa hapa. Hata hivyo kwa muda wa miezi kadhaa iliyopita kampuni yetu imekuwa ikisimamia mradi wa kuihamasisha jamii kuhusu uhifadhi wa mazingira.
8. **Roland:** Mpango mzuri huo!
9. **Zakia:** Tunawapa mafunzo na kisha tunawaomba wajitolee kulinda hilo eneo .
10. **Roland:** (**Agreeing**) Alaa! Hivi, umekuwa ukifanya kazi afisini kwenu kwa muda gani?
11. **Zakia:** Miezi kumi na mmoja. Ni kazi yangu ya kwanza.

12.**Roland:** Umesomea kipi kinachohusiana na kazi yako?

13.**Zakia:** Urithi na utalii. Hivi sasa ninasomea masuala ya mawasiliano.

14.**Roland:** Na... Umeolewa?

15.**Zakia:** (**Firmly**) Hilo ni suala la binafsi na sijaridhia kulijibu..

16.**Roland:** Samahani! Ninapokutazama u mdogo na umekoma kiakili – ndiposa nikataka kukufahamu zaidi...

17.**SFX ATMO : MOBILE PHONE RINGS – STEPS ON DEAD LEAVES AND TWIGS**

18.**Zakia:** Niwie radhi! Naomba nipokee hii simu (**Walking away**) Hallo?

19.**Elinam:** (**on the phone**) Hallo!

20.**Zakia:** (**Shouting**) Oh hallo Elinam! (**Shouting at Latifa**) Latifa, njoo hapa, ni kakako! (**On the telephone**) Hujambo?

21.**Elinam:** Sijambo. U hali gani, Zakia?

22.**Zakia:** Sijambo! Kwani mambo yalikwendaje siku ile?

23.**Elinam:** Samahani sana, Zakia. Ilinibidi kuandaa makala ya kuwasilisha katika chuo kikuu. Mambo yalikuaje?

24.**Zakia:** Nitampa nafasi Latifa akusimulie yeye mwenyewe.

25.**Elinam:** Mpe simu basi!

26.**Latifa:** Mambo vipi Elinam!

27.**Elinam:** Mambo poa, dada. Najaribu kukisia lakini sijafanikiwa. Ebu nambie!

28.**Latifa:** Nilipita mtihani!

29.**Elinam:** (**He shouts**) Hongera! Nilijua vizuri kwamba ungepita! Hongera mdogo wangu!!

30.**Latifa:** Asante sana!

31.**Elinam:** Na... Wajua hali ya mambo hapa?

32.**Latifa:** Hapana...

33.**Elinam:** Nimepata fedha za ufadhili!

34.**Latifa:** Kweli?

35.**Zakia:** Kasema nini? Imekuaje?

36.**Latifa:** Hatimaye amepata fedha za ufadhili!

- 37.**Zakia:** (**Shouting**) Bahati iliyoje!!! Elinam, bora uje wakati wa likizo ili tupate kusherehekea pamoja!
- 38.**Elinam:** Latifa! Je ungependa kufanya mtihani wa wanafunzi wanaotaka kuwa madaktari wasaidizi?
- 39.**Zakia:** Hasa masomo hayo yana umuhimu gani?
- 40.**Elinam:** Utasoma masomo ya utabibu kwa muda wa miaka mitatu, kisha utakuwa daktari msaidizi. Tuseme ni daktari mdogo!
- 41.**Latifa:** Unadhani masomo hayo yatanifaa?
- 42.**Elinam:** Uamuzi ni wako wewe. Lakini unapaswa kuzingatia faida zake kifedha na pia nafasi za kazi. Unaonekana kwamba unayamudu vizuri masomo ya sayansi na hospitali zetu zinahitaji wahudumu...Sekta nyingine zinakabiliwa na hali ngumu.
- 43.**Latifa:** Ninahitaji muda wa kiasi gani kuliwazia hilo?
- 44.**Elinam:** Huna muda mwingi! Mtihani wenyewe utafanywa wiki mbili zijazo na unatakikana ujisajili siku tatu kabla.
- 45.**Latifa:** Sawa. Mbona usinipigie simu tena kesho? Tutakuwa pamoja na Zakia.
- 46.**Elinam:** Haya, Nitawasiliana nanyi hapo kesho!
- 47.**Latifa and Zakia:** Tutawasiliana kesho! (**They hang up laughing**)

48. **Zakia:** Latifa, usiliwaze sana kila wakati. Jaribu hilo uliloambiwa. Endapo hukulipenda somo hilo utasoma chengine baadaye ukitaka!
49. **Latifa:** Nilitaka kwanza nipate ushauri wako.
50. **Zakia:** Lau ingekuwa wazazi wako wote wanakuunga mkono, ungeendelea na masomo mpaka kiwango ukitakacho wewe. Lakini inakubidi ufuata njia za mkato ili usije ukaendelea kupata misukosuko ambayo hukuitarajia.
51. **Latifa:** Umesema kweli Zak, nitaufanya huo mtihani. Aah! Nadhani watalii wamechoka kusubiri...
52. **Zakia:** Kweli, twen'zetu!
53. **SFX ATMO:** Steps (two women) running on dead leaves and twigs
54. **NARRATOR:** *Baada ya ziara yao mlimani, Latifa, Zakia na watalii wanaondoka kuelekea kwenye mji mdogo. Watalii wanavutiwa na maeneo wanayoyatembelea kila siku. Mtihani wa madaktari wasaidizi unafanyika kote nchini, kwa hivyo Latifa ataweza kuufanyia katika mji wao mdogo. Anafurahi sana anapogundua kwamba yumo kwenye orodha ya wanafunzi waliopita. Baadaye kidogo, Mamoua anajifungua mtoto wa kike na Latifa anakatiza mipango yake ili amsaidie mama yake. Baada ya muda usio mrefu, unafikia wakati wa Latifa kuhamia kwenye mji mkuu kiliko Chuo cha Madaktari Wasaidizi. Lakini siku moja asubuhi mlima wa volkeno unaripuka karibu na nyumbani kwa Papa Wali.*

Scene 2, AT PAPA WALI'S HOME

Papa Wali, Mamoua na Latifa

55. SFX ATMO: HENS CLUCKING IN THE BACKGROUND. SOME SHEEP BLEET – SOME TRAFFIC IN THE DISTANCE

56.Papa Wali: (angry) Latifa, unataka nini? Unataka kutuagamiza?

57.Latifa: Sikuelewi baba?

58.Papa Wali (angry) Ulihakikisha kwamba umerejea shule badala ya kukaa nyumbani kumsaidia mamako wala hakuna aliyesema chochote. Ulipita mtihani wako kama ulivyokuwa ukitaka. Sasa hivi mama yako amejifungua mtoto mwingine, una lazima ya kuondoka ukaishi na kakako na kujiunga na Chuo cha Madaktari Wasaidizi.

59.Mamoua: (Playing the victim) Biashara ya uji unayoidharau ndiyo iliyokulisha katika nyumba hii; ndiyo iliyokuvisha na kukununulia vifaa vya shule... na leo unathubutu kutuambia kuwa hatma yako haitegemei uji! (Shouting) Latifa!!!

60.Latifa: Baba, Lakini ninakwenda kuishi pamoja na Elinam' ili nisome masomo ambayo siwezi kuyapata hapa mjini kwetu!

61.Papa Wali: Masomo yote yaliyomo katika mji huu umeyapuuza kisha umefuatia somo ambalo huwezi kulisoma hapa mjini kwetu, Latifa!

62.Latifa: Elinam ndiye aliyenishauri kufanya hivyo.

63.Papa Wali: Elinam amekuwa baba yako sasa? Akirudi hapa nyumbani atanitambua mimi ni nani, hilo ninakuhakikishia!

64.Latifa: Hakuna aliyelalamika wakati alipoondoka. Ikizidi alifungashiwa kila kitu alichohitaji!

65.Mamoua: Elinam ni mvulana! Akijaliwa kupata kazi atarejea nyumbani pamoja na mke wake, Mungu akipenda! Atahakikisha kuwa ametusimamia kwa kila hali na mke wake atanisaidia kufanya kazi za nyumbani. Lakini wewe Latifa, usiponisaidia leo, utanisaidia lini? Utakapokuwa kwa mume wako ukimtunza pamoja na wazazi wake?

66.Latifa: Mama, sihitaji chochote kile, kwa masomo yangu, au hata kodi ya nyumba pamoja nafedha za chakula. Naomba mniruhusu kwenda mjini ili nijiandae katika maisha yangu ya baadaye.

67.Mamoua: Ehe, nipishe mbali! Mimi ndiye sijafaulu maishani eee, siyo? Nani amekufurisha kichwa hivyo? Huyo rafiki yako?

68.Latifa: Baba, naamini unanielewa. Niunge mkono tafadhali na umweleze ili naye afahamu?

69.Papa Wali: Nikuunge mkono kisha niseme kitu gani?Wewe hujifanyia mambo unavyotaka? Hata huombi ruhusa. Unatujulisha tu kwa kuwa mwenyewe ushajiamulia utakalo.

70.Latifa: (With tears in her eyes) Naomba baraka zenu, baba.

71.Papa Wali: Ulitaka radhi yetu kabla ya kufanya mtihani wako au huu wa kujiunga na chuo cha madaktari?Jee ulitufahamisha kwamba utafanya huo mtihani?

72.Latifa: Samahani, baba, lakini nilichelea kwamba hamngeniruhusu.

73.Papa Wali: Sasa basi mbona utujulishe sasa? Na je nikisema “hapana”?

74.Latifa: (Silence) ...

75.Papa Wali: Bila shaka, kauli zangu hazingekuwa na maana yoyote maana ungefunganya mizigo yako na kuondoka.

76.Latifa: (**Crying loudly**) Baba...Ninataka nifaulu ili nipate kuwasaidia katika siku za usoni...

77.Mamoua: Huna haja ya kulia sasa! Utayahitaji machozi yako wakati mwanao atakapokuwa akikutenda haya unayonitenda mimi!

78.Papa Wali: (**realizing they went too far**) Mamoua, kauli gani hizo ? Unamlaani binti yako?

79.Mamoua: Anafaa nini kingine ila hicho?

80.Papa Wali: (**firmly**) La hashu! Ila hilo! Hata kama si mtiifu lakini tunapaswa kujivunia mafanikio yake! Amekusaidia mpaka sasa lakini hivi unamuona sawa na takataka kwa kuwa anataka kuondoka! Naona umevuka mipaka!

81.Mamoua: Nani atakayeshughulikia usafi hapa nyumbani kama si yeye? Unadhani mimi ndiye nitakayefua vibinda vya mtoto?

82.Papa Wali: Nitafanya mwenyewe, wala si tatizo. (**To Latifa**) Latifa!

83.Latifa: Beeh,?

84.Papa Wali: Una ruhusa ya kwenda! Funganya mizigo yako na mimi nitakusindikiza hadi kwenye kituo cha mabasi utakapokuwa tayari kuondoka.

85.Latifa: Asante sana, Baba... (**She leaves the room discreetly**)

86.Papa Wali: Naondoka. Nina kazi ya kufanya. (**Gets up**)

**87.SFX ATMO: SOUND OF METAL CHAIR SCRAPING THE FLOOR.
FOOTSTEPS (ONE MAN) GOING AWAY**

88.Mamoua: Hayo ndiyo ya kuniambia mimi? (**Angrily**) Wali! Tutaona hali yake atakapokuwa mjamzito! (**For FADE OUT**)... Hilo ndilo atakalofaidi atakapokwenda jijini... na wahuni wote hao walio jijini wanaowalaghai wasichana wa vijijini wasioelewa mambo...

MUSIC

OUTRO

Baada ya siku tatu zilizofuatia, Latifa aliondoka kuelekea jijini ambako kakake Elinam alikuwa akimsubiri. Rafiki yake wa dhati, Zakia alitokwa na machozi alipokuwa akimsindikiza kwenye kituo cha mabasi. Babake naye alishindwakuzuwia hisia za huzuni. Mamoua hakuwepo..

Alipofika jijini, Latifa akaanza kuishi nyumba moja na kakake na wakati huo huo akajiunga na Chuo cha Madaktari Wasaidizi.

Je mambo yatakwenda sawa? Atakuwa salama kwenye harakati za jijini? Ili kufahamu zaidi, sikiliza sehemu itakayofuata ya “Mtoto wa kike ahitimu shule”, katika mfululizo wa makala inayoelezea elimu na kutojua kusoma na kuandika.

Ukitaka kukisikiliza tena kipindi hiki au vyengine vya mfululizo wa Noa Bongo-Jenga Maisha Yako, tizama ukurasa wetu wa wavuti www.dw-world.de/lbe.

Unaweza pia kutuandikia barua-pepe kupitia anwani: lbe@dw-world.de

Shukran kwa kutusikiliza! Hadi wakati mwengine nakutakia wakati mwema!!

END OF 6th EPISODE